

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE

27 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE TAREHE 27 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika
Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**439. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itahakikisha kunakuwa na maeneo
maalum ya Watu wenye Ualbino kwenye mikutano
ya hadhara ili wasikae juani.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

440. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Nandembo - Kitula hadi Nampungu - Tunduru kwa kiwango cha lami.

441. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini fedha za kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Mji wa Mhunze Wilayani Kishapu kwa kiwango cha lami zitatolewa.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

442. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itamaliza kulipa madeni ya muda mrefu ya Watumishi.

WIZARA YA NISHATI:

443. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, makubaliano ya mkataba ujao kati ya SONGAS na Serikali yamefikia hatua gani ikiwa mkataba wa awali upo katika mwaka wa mwisho.

444. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itarejesha gharama za kuunganishiwa umeme kuwa 177,000/=.

WIZARA YA MAJI:

445. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mabwawa ya maji ya Salama A, Rakana, Mihingo, Tingirima, Kambubu na Nyaburundu - Bunda.

WIZARA YA AFYA:

**446. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, Wodi ya Watoto na Wodi ya Wanaume Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi utakamilika.

**447. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA
(ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia Watoto kupata matibabu baada ya kufuta Toto Afya Kadi huku tukisubiri Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

**448. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Kampeni ya kunawa mikono ili kudhibiti magonjwa ambukizi.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA
YA HABARI:**

449. MHESHIMIWA MUSSA OMAR SALIM (GANDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali haioni haja ya kuhamishia Mfumo wa *Cyber* kuwa chini ya udhibiti wa Jeshi la Polisi.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**450. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, upi Mkakati wa Serikali kuhakikisha Wajasiriamali wadogo wanakuwa sehemu ya Wawekezaji wa ndani kupitia shughuli zao.

WIZARA YA UJENZI:

**451. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR
(NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Ujenzi wa Barabara ya Kharumwa yenye Urefu wa Kilomita 1 kwa kiwango cha Lami utakamilika.

WIZARA YA FEDHA:

452. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna Kampuni ngapi nchini za kutoa Taarifa za Mikopo (*Credit Reporting Company*) zinazoangalia hali ya kifedha ya mkopaji na uwezo wake wa kulipa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
27 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**